**/"Learning by Ear – Climate Change**

**Episode 09**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli:Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- MR GITAKI – ENVIRONMENT MINISTER (61)
- MRS CHRISTINE KIMASI – RENEWABLE ENERGY INVESTOR (50)
- LORNA (16)
- CAROL (14)
- JOSHUA (15)
- ALEX (15)

Scene 2:

- ALEX (15)
- JOSHUA (15)
- CAROL (14)

- LORNA (16)

Scene 3:

- MR GITAKI – ENVIRONMENT MINISTER (61)
- MR KAPOOR – NATIONAL POWER BOARD (60)
- MRS CHRISTINE KIMASI – RENEWABLE ENERGY INVESTOR (50)
- LORNA (16)
- CAROL (14)
- JOSHUA (15)
- ALEX (15)

**Intro:**

Hujambo na karibu kwa makala mengine ya “Noa Bongo Jenga Maisha yako” mchezo wa redio kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa. Katika kipindi cha leo, Waziri wa mazingira aingilia kati kulisaidia jopo kazi la wanafunzi wanaopinga ujenzi wa kiwanda cha umeme mjini Dhowvville. Je bodi ya taifa ya umeme iko tayari kufanya mazungumzo na jopo kazi kuhusu njia bora za kuepusha mabadiliko ya hali ya hewa? Endelea kuwa nasi hadi mwisho ufahamu mengi zaidi katika makala haya!

## Scene One: Ministry of Environment

| | |
|---|---|
| **SFX ATMOS:** | **OFFICE/CHATTER/PHONES RINGING** |
| **1. ALEX:** | Singejali kuwa waziri kama mambo ni haya. Mtu anapewa ofisi kubwa namna hii. Hebu tazama, televisheni na friji pia! |
| **2. CAROL:** | Alex,hii ndio sababu tuko na viongozi bure kabisa hapa nchini. Wanachojali ni maslahi yao tu. Kama wanawake wengi zaidi wange….. |
| **3. MRS KIMASI:** | Shhh, Carol! Nafikiri waziri karibuni atawasili na tunapasa kuonekana watu wa nidhamu na kuheshimika wanaojua wanachofanya.. |
| **SFX:** | **(OPENING DOOR)** |
| **4. MR GITAKI:** | Habari za asubuhi nyote?. Ahh sidhani tumekutana na wengine wenu...! |

| | |
|---|---|
| **5. MRS KIMASI:** | Naitwa Christine Kimasi. Mimi ni mwekezaji katika sekta ya nishati inayoweza kutumika tena na tena na inayozingatia usafi wa mazingira. Tunashirikiana na jopo kazi kutafuta njia bora za kuzalisha kawi isiyochafua mazingira. |
| **6. MR GIATKI:** | Vyema kabisa! Wewe ndiye mtu tunayehitaji zaidi katika mpango huu. Mfanyabiashara….! |
| **7. MRS KIMASI:** | Sawa, lakini heshima zangu ni kwa jopo kazi hili. Mimi niko hapa kupata ufadhili na kuungwa mkono. |
| **8. MR GITAKI:** | Kwa hivyo kwa maoni yako ni njia gani bora na salama kwa tatizo la umeme mjini Dhowville? |

**9. MRS KIMASI:** Tuko na njia tatu,- uzalishaji wa nishati kupitia mimea, maji au upepo.

**10. MR GITAKI:** Mmm, nishati inayotokana na upepo. Hivi majuzi nimehudhuria kongamano nchini Misri lililojadilia uwezekano wa kutumia upepo kuzalisha kawi barani Afrika.

**11. LORNA:** Nchini Misri? Wanatumia nishati inayotoaka na upepo huko?

**12. MR GITAKI:** Ndiyo, Misri ni miongoni mwa mataifa yanayotoa kiasi kikuba cha nishati barani Afrika kwa kutumia upepo. Viwanda hivi vinapatikana katika jangwa la Sahara. Wametumia aina maalum ya matabo ya upepo yanayoweza kustahamili joto kali na ukame. Njia hii ni muhimu na inatumika sana miongoni mwa mataifa ya kaskazini mwa Afrika.

**13. CAROL:** Lakini inafanya kazi vipi?

**14. MRS KIMASI:** Nishati inayotokana na upepo ni salama, inaweza kutumika tena na tena na haichafui mazingira.

**15. CAROL:** Kwa hivyo tunaweza kuanzisha mradi wa aina hiyo hapa Dhowville?

**16. MRS KIMASI:** Inawezekana…ingawa hakuna upepo mwingi wa kutosha kutosheleza mahitaji ya mji au nchi nzima kwa jumla!

**17. MR GITAKI:** Pia lazima tufikirie iwapo wakaazi wa mji huu watakubali kuwa na matabo makubwa ya upepo. Yayaweza kusababisha usumbufu.

**18. MRS KIMASI:** Kabla ya kufikiria gharama ya kuwekeza au kujenga matabo haya. Mwekezaji anaweza kusita kuweka rasilimali zake katika mradi wa aina hii, endapo wakaazi wataupuuza na kushindwa kutunza matabo hayo.

**19. JOSHUA:** Lakini nafikiri punde tu matabo hayo yatakapojengwa, umeme unaotokana na upepo lazime uwe wa gharama nafuu, sivyo?

**20. MRS KIMASI:** Ndio Joshua, ni wa gharama nafuu sana kwa sababu punde tu unapoweka matabo, huhitaji mafuta kuendesha mitambo. Ni upepo tu unaotumika kuzalisha nishati hiyo. Jukumu kubwa ni kutafuta eneo linalofaa lenye upepo mkali kwa mradi huo - basi!..

**21. MR GITAKI:** Sawa, hatua nyingine – kupanga mkutano na bodi ya taifa ya umeme nchini kujadilia suala hili?..

**22. MRS KIMASI:** Ndio, na tayari nimeanza kuzungumza na baadhi ya wajasiriamali ambao wako tayari kufadhili miradi ya aina hii.

| | |
|---|---|
| **23. MR GITAKI:** | Pia nimezungumza na bwana Kapoor kutoka bodi hiyo. Amekubali tukutane naye kesho asubuhi. Nimemwambia kwamba pia nitaandamana na kundi la washauri, na kundi hilo ni nyinyi hapa. |
| **24. CAROL:** | Hatimaye wamekubali tukutane nao. |
| **25. MR GITAKI:** | Ok, sawa basi tukutane kesho saa nne asubuhi. |
| **26. ALL:** | Asante sana mheshimiwa, tukutane kesho! |
| **SFX:** | **(SCRAPING CHAIRS)** |

**Scene Two: Just outside Dhowville**

| | |
|---|---|
| **SFX ATMO:** | **CITY NOISES** |
| **27. JOSHUA:** | Alex, unatupeleka wapi? |
| **28. ALEX:** | Nimefurahishwa sana na wazo la bibi Kimasi kuhusu uzalishaji wa nishati inayotumia upepo, na tayari najua mahali pa kujenga na kuweka matabo ya mradi huo. |

| | |
|---|---|
| **29. CAROL:** | Kweli? Wapi? |
| **30. ALEX:** | Ndio nataka kumuonyesha. |
| **SFX:** | **SLUM AREA CHICKENS/PEOPLE/MUSIC** |
| **31. JOSHUA:** | Nyumba yangu ile pale. Unataka kutupeleka msituni kwenye milima nje kabisa ya mji? |
| **32. ALEX:** | Ndio, kupita ule mtaa wa mabanda. Hapo kuna eneo zuri linalofaa kabisa kuweka matabo ya upepo.. |
| **33. CAROL:** | Wacha mzaha Alex? |
| **34. ALEX:** | Si mzaha, hilo ndilo eneo lenye upepo mwingi zaidi hapa Dhowville. |

| | |
|---|---|
| **35. LORNA:** | Lakini Alex, ina maana tukate msitu wote. Huo ni uhalifu mkubwa na kinyume kabisa na juhudi zetu za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa! |
| **36. ALEX:** | Una maana gani? |
| **36. CAROL:** | Miti ni muhimu….ni muhimu kwa sababu inasaidia kuhifadhi mazingira bora na kudumisha hali nzuri ya hewa. |
| **37. JOSHUA:** | Ndio Carol. Miti husaidia kuondoa dioksidi ya kaboni angani na kuihifadhi kwenye majani, shina na hata kwenye mizizi ardhini**.** |
| **38. CAROL:** | Kwa hivyo wakati miti inapokatwa au kuharibiwa, dioksidi hii ya kaboni huachiliwa hewani na kuchangia mabadiliko ya hali ya hewa. |

**39. JOSHUA:** Ni kweli nimesoma kwamba uharibifu wa misitu huchangia asilimia 20 ya kaboni inayotolewa angani na hivyo kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa. Kuna kiwango kikubwa cha kaboni inayotokana na ukataji wa miti kiholela kama vile nchini Brazil, Argentina na Indonesia.

**40. ALEX:** Josh, sikuwa na habari!

**41. JOSHUA:** Misitu yetu inayoleta mvua barani Afrika hutekeleza jukumu muhimu la kuchuja dioksidi ya kaboni angani. Hivyo basi tunahitaji sana misitu hii!

**42. LORNA:** Nadhani tunaweza kusema misitu mikubwa huwa kama maeneo yanayozuia mabadiliko ya hali ya hewa.

| | |
|---|---|
| **43. CAROL:** | Alex, hebu fikiria aina zote za wanyama wanaoishi msitu. Wote wangekufa! Na hata mimea ambayo... |
| **44. ALEX:** | Sawa tosha! Nilifikiri misitu ni kwa matumizi ya kuni na mashamba ya binadamu. |
| **45. LORNA:** | Hapana! Ndio sababu watu wana hofu ya kuangamia kwa msitu wa Amazon au ule unaopatikana nchini Kongo. Misitu hii ni muhimu sana na inapoharibiwa ni vigumu kuirejesha. |
| **46. ALEX:** | Kweli sikuwa na habari. Je upo uwezekano wa kupanda misitu iliyoharibiwa? |
| **47. CAROL:** | Ndio unaweza kunasa kaboni kwa kupande tena miti mahali ilikokatwa. Misitu mipya kisha huchuja dioksidi ya kaboni kutoka angani na kuhifadhi kaboni hiyo kwenye majani, mashina na mizizi yake ardhini pia. |

| | |
|---|---|
| **48. JOSHUA:** | Lakini, Carol, bado kuna tatizo - hebu tazama msitu ule pale - fikiria aina mbalimbali ya miti na wanyama wanaoishi katika msitu huo. |
| **49. CAROL:** | Ehhhe, sasa tatizo liko wapi? |
| **50. JOSHUA:** | Tatizo ni kwamba unapopanda tena msitu kuna hatari ya kukuza aina moja ya mti ,na huenda aina nyingine ya mimea ikazuiwa kukua na hivyo kuchakaza mbolea ardhini.. Kama vile wakulima wanapopanda mahindi katika mashamba yao kwa muda mrefu. |
| **51. CAROL:** | Sawa. Kwa hivyo una maana kwamba ni lazima uiangalie vyema misitu kama vile mkulima anavyofanya,kuweka mbolea, na madawa ya kuua wadudu shambani mwake…..? |

| | |
|---|---|
| **52. JOSHUA:** | Hasa, wajua endapo miti hiyo itavamiwa na wadudu, basi huenda msitu wote ukaangamia. Huwezi kupata ule utajiri wa kiasilia wa misitu iwapo utapanda aina moja tu ya mti kama vile mti wa msonobari au mkalitusi. |
| **53. ALEX:** | Inaonekana inaweza kuwa na athari zaidi kuliko ukataji wa misitu. |
| **54. JOSHUA:** | La hasha. Unajua kila mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa zina manufaa na athari zake. Cha msingi ni kutafuta njia bora zisizo na athari kubwa zaidi. Hebu twende, mbu wanazidi kutufyonza! **(swotting mosquitoes)** |

**Scene Three: Dhowville Local Government Office**

| | |
|---|---|
| **SFX ATMO:** | **OFFICE RECEPTION** |

**55. MR GITAKI:** **(walking & talking)** Ni jambo la busara sana kuhudhuria kwako mkutano huu bwana Kapoor.

**SFX:** **LIFE DOORS OPENING & CLOSING**

**SFX ATMO:** **INSIDE LIFT**

**56. MR GITAKI:** Unajua, serikali imejitolea kuhakikisha kuwa wananchi wengi zaidi wanapata huduma za umeme. Na ni jukumu langu kuona kwamba tunafanikisha lengo hili kwa kutumia nishati inayoweza kutumiwa tena na tena na inayozingatia usafi wa mazingira.

**57. MR KAPOOR:** Ni kweli mheshimiwa, lakini ni lazima tuzingatie vipi tunaweza kufanya biashara nzuri na pia…

**SFX:** **LEFT BELL & DOORS OPEN**

**58. MR GITAKI:** **(Walking & Talking)** …Na ndio sababu nilimuuliza mjasirimali wa sekta ya nishatii akiandamana na washauri wake kuhudhuria mkutano..

**SFX:** **(OPENING DOOR)**

**59. MR GITAKI:** Ndio hawa hapa wamefika! Ningependa kumjulisha kwa bwana Kapoor kutoka bodi ya taifa ya nishati nchini. Na bwana Kapoor huyu hapa ni Bi Christine Kimasi mtaalam na mwekezaji katika sekta ya nishati inayoweza kutumika tena na tena na isiyochafua mazingira. Na hawa ni wanachama wa jopo kazi na washauri…. kwanza kabisa ni Bi Lorna, Carol, Alex na Joshua. Labda pengine umewahi kuwasikia.

**60. MR KAPOOR:** Hawa vijana wanajaribu kupinga mradi huu! Sasa wanafanya nini katika mkutano huu?

**61. MR GITAKI:** Kama nilivyotangulia kusema, nishati inayoweza kutumika tena na tena na isiyochafua mazingira, ndio suluhisho na salama kwa siku za baadaye, na vijana hawa wamekumbatia wazo!

**62. MRS KIMASI:** Na hiyo itaokoa na kuimarisha biashara yako na yangu pia siku za usoni!

**63. MR KAPOOR:** Sina muda mwingi hapa, kwa hivyo nadhani tunaweza kuanza mazungumzo yetu mara moja. Kawaida mimi sina muda wa kupoteza na vijana kama hawa ambao ni waharibifu na watovu wa nidhamu.

**65. CAROL:** Ok! Sawa bosi. Hapa kuna njia tatu, zinazoweza kutatua shida ya umeme katika mji huu wa Dhowville. Ni bora na salama zaidi zisizochafua mazingira. Tunataka kuzuia kiwanda hiki kipya kutoa gesi na moshi unaochafua mazingira na kuchangia katika mabadiliko ya hali ya hewa. Suala la mabadiliko ya hali ya hewa ni tatizo kubwa hapa barani Afrika.

**END OF EPISODE 9**

**Outro:**

Na hadi hapo msikilizaji tunafika mwisho wa kipindi cha leo. Ungana nasi tena kwa kipindi cha kumi na cha mwisho kuhusu suala la mabadiliko ya hali ya hewa. Je bodi ya taifa ya kawi itabadili msimamo wake na kushirikiana katika juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa au itaendelea kushikilia msimamo wake wa kutumia mafuta yanayochafua mazingira? Mchezo huu umeandikwa na Victoria Averill. Na kumbuka ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki, tembela mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa na asante kwa kutusikiliza!